



MAMLAKA YA UDHIBITI WA  
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI  
(EWURA)



**TANGAZO KWA UMMA**

**MWITO WA KUPATA MAONI YA WADAU KUHUSU UTAFITI WA GHARAMA  
ZA UENDESHAJI ZA WAUZAJI WA MAFUTA WA JUMLA NA REJAREJA**

Mwaka 2019, Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ilitafuta mshauri mwelekezi ili atengeneze mfumo wa kukokotoa faida stahiki ya wauzaji wa mafuta kwa jumla na rejareja. Ili kufanikisha hilo, mshauri mwelekezi alitakiwa kubainisha gharama halisi za uendeshaji pamoja na faida inayokubalika. Sababu kubwa za kufanya utafiti huu ni:

- i) utafiti wa kwanza ulifanyika mwaka 2013, ambapo gharama zimedilika kutokana na fahirisi ya bei ya walaji isiyo ya chakula
- ii) kufanya mapitio ya gharama za usafirishaji wa mafuta kutoka katika maghala ya kuhifadha mpaka katika vituo vya Mafuta. Gharama hizo zilipangwa mwaka 2009 kuwa Shilingi 10/lita kwa Dar es salaam na
- iii) kujumuisha gesi ya kupikia (LPG) kwenye mfumo wa uagizaji mafuta kwa pamoja kama ilivyobainishwa kwenye Kanuni za Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja.

Kwa mujibu wa Kifungu Na. 19 (2) cha Sheria ya EWURA Na. 414, EWURA imeanzisha mchakato wa kupata maoni ya wadau kuhusiana na taarifa ya utafiti wa gharama za uendeshaji za wauzaji wa jumla na rejareja wa mafuta. EWURA itakusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Kampuni za Mafuta (OMCs); Wauzaji Mafuta kwa Rejareja; Baraza la Wawakilishi wa Watumiaji wa Huduma zinazodhibitiwa na EWURA (EWURA CCC); Baraza la Ushauri la Serikali (GCC) pamoja na wananchi kwa ujumla.

Mkutano wa taftishi wa kukusanya maoni kutoka kwa wadau utafanyika katika **Ofisi za EWURA Kanda ya Mashariki, Ghorofa ya 7, Jengo la PSSSF (zamani LAPF), Barabara ya Bagamoyo, tarehe 23 Desemba 2020 kuanzia saa nne kamili asubuhi**. Wadau wanaopenda kutoa maoni yao kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kumwandikia Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyoonyeshwa hapo chini kabla ya tarehe **31 Desemba 2020**. Wadau watakaopenda kupewa muda wa kuwasilisha maoni yao katika mkutano wa wadau wanatakiwa kuonyesha nia yao kwa kuiandikia EWURA kabla ya tarehe **21 Desemba 2020**.

Taarifa ya utafiti inapatikana katika tovuti ya EWURA. Nakala za taarifa hiyo zinapatikana pia katika ofisi za EWURA wakati wa muda wa kazi kuanzia saa **2.00 asubuhi** mpaka saa **10.00 jioni**. Wadau wanaombwa kuzingatia muda

uliopangwa wa kutoa maoni ili kufanikisha zoezi hili. Ufafanuzi zaidi unaweza kupatikana kwa kumwandikia Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyotajwa hapo chini.

**Limetolewa na:**

**Mkurugenzi Mkuu  
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**

**17 Desemba 2020**